# JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA SAME

**FAHARI YA SAME**

**Maendeleo Daima**

**Toleo la Desemba,2025 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz SAME DC samedc2022**

## SALAMU KUTOKA KWA MKURUGENZI



***Bw.Jimson Mhagama-Mkurugenzi Mtendaji-Same***

***Wazazi andikisheni Watoto shule, na wa Kidato cha kwanza wote waripoti shuleni***

*Nawatakia heri ya Mwaka Mpya 2026 Wananchi wote wa Wilaya ya Same. Mwaka 2025 umemalizika salama na ninashukuru kwa ushirikiano mkubwa mlioutoa kwa Serikali katika kuhakikisha kuwa masuala mbalimbali ya maendeleo yanasonga mbele.*

*Msimu wa sherehe mbalimbali za mwisho wa mwaka tumeumaliza, napenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha tena kwenye ujenzi wa Taifa letu la Tanzania. Napenda kuwakumbusha ndugu zangu wa Wilaya ya Same kwamba jukumu kubwa liliopo mbele yetu kwa sasa ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza wanaripoti shuleni bila kukosa.*

*Kwenye Wilaya yetu ya Same Jumla ya wanafunzi 4,305 wamechaguliwa kujiunga na elimu ya Sekondari mwaka 2,026, kwahiyo wanafunzi wote waliochaguliwa tunataka kuwaona shuleni.*

*Kwa kutambua kuwa elimu ni msingi bora wa maisha ya mtoto tayari wilaya inayo shule na madarasa ya kutosha kupokea wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na Sekondari. Tukumbuke kuwa Serikali inatekeleza Sera ya Elimu bure ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata fursa ya kupata elimu bila kuwa na kisingizio chochote, hivyo hakuna sababu ya mzazi kutompeleka mtoto shule.*

*Niwakumbushe pia wazazi wenye watoto wenye umri wa kuanzia miaka mitano kuhakikisha kuwa wanawaandikisha darasa la awali na darasa la kwanza, uandikishaji umeanza mwezi Desemba 2025 na utakamilika Machi 31, 2026.*

*Serikali imetoa muda wa kutosha kwa wazazi kuhakikisha kuwa wanawaandikisha kuanza darasa la kwanza watoto wote wenye umri wa kwenda shule, wazazi mtambue kuwa ni kosa kutompeleka mtoto shule.*

*Kila mtoto ana haki ya kupata elimu hivyo kila mzazi atimize wajibu wake wa kuhakikisha kuwa anampeleka mtoto shule na pia kuhakikisha anafuatilia maendeleo ya mtoto wake shuleni.*

*Mwaka huu tunatarajia kuandikisha wanafunzi 5,256 darasa la awali na wanafunzi 5,542 darasa la kwanza na hadi kufikia Januari 23, 2026 kwa darasa la kwanza tumefikia asilimia 96 ya uandikishaji na darasa la awali tumefikia asilimia 105.*

*Elimu ni ufunguo wa maisha, Mzazi hakikisha unampatia mwanao ufunguo.*

**SAME YAPATIWA GARI LA ZIMAMOTO**




***Gari la zimamoto lililokabidhiwa Wilayani Same kwaajili ya kusaidia kupambana na majanga ya moto.***

Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuipatia Wilaya hiyo gari la zimamoto.

Mheshimiwa Kasilda ametoa shukrani hizo wakati akikabidhiwa gari hilo na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mheshimiwa Nurdin Babu ambapo alisema Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kuimarisha usalama wa wananchi.

Akikabidhi gari hilo Mkuu wa amkoa wa Kilimanjaro Mheshimiwa Babu amewataka Viongozi wa Wilaya ya Same kuhakikisha kuwa gari hilo linatunzwa ili liweze kukabiliana na majanga ya moto kwa muda mrefu.

Kwa mwaka huu pekee Wilaya ya Same ilishuhudia ajali mbaya kabisa ya Moto baada ya magari mawili ya abiria kugongana na kuweka Moto ajali ambayo ilipoteza maisha ya watu zaidi ya 40 na ajali nyingine za Moto zilizotokea ni kuungua kwa mabweni ya Wanafunzi kwenye Shule za Sekondari Bemko na Makanya.

## DC SAME AMWANGUKIA WAZIRI ULEGA KUOMBA UJENZI WA BARABARA YA SAME-SIMANJIRO

Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe. Kasilda Mgeni, amemwomba Waziri wa Ujenzi, Mhe. Abdallah Ulega, kutenga fedha kwaajili ya kujenga barabara na daraja linalounganisha Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro na Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara.

Mhe. Kasilda ametoa ombi hilo wakati Waziri Ulega alipotembelea Wilaya ya Same kukagua Miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja inayoendelea Wilayani Same.

Akijibu ombi hilo, Waziri wa Ujenzi Mhe. Abdallah Ulega, alisema Serikali imelipokea na itaweka utaratibu wa kulijumuisha katika mpango wa bajeti ijayo ya 2026/2027 ili utekelezaji wake uweze kuanza.

## KATA YA HEDARU YAISHUKURU SERIKALI KUJENGEWA DARAJA LA WASHI



***Daraja la Washi lililopo Kata ya Hedaru***

Wakazi wa Kata ya Hedaru, Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, wameishukuru Serikali kwa kutoa fedha zaidi ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Mto Washi.

Ujenzi wa daraja hilo umemaliza changamoto sugu ya mafuriko yaliyokuwa yakisababisha vifo vya watu, uharibifu wa mali, mazao na kukatika kwa mawasiliano ya barabara kati ya mikoa ya Kilimanjaro na Tanga.

Wananchi hao wametoa shukrani zao kwa Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni alipotembelea na kukagua ujenzi wa daraja hilo.

Mhe. Kasilda alieleza kuridhishwa na kazi iliyofanywa na TANROADS, huku akimpongeza Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Ujenzi kwa dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha miundombinu ya barabara na kuondoa changamoto mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili wananchi.

“Mradi huu umetumia fedha nyingi za Serikali zaidi ya shilingi bilioni 1.5 hivyo ni wajibu wa kila mwananchi kuutunza na kuilinda kwa wivu mkubwa.

Bw.Rajab Msheri Mkazi wa Hedaru anasema daraja hilo ni mkombozi mkubwa kwao kwani limeondoa hatari ya mafuriko yaliyokuwa yakisababisha vifo, uharibifu wa mali na kukatika kwa mawasiliano ya barabara kati ya mikoa ya Kilimanjaro na Tanga.

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa TANROADS Mkoa wa Kilimanjaro ambaye pia ni Mhandisi Mkazi wa mradi huo, Mhandisi Benitho Mnzovela, amesema mradi umekamilika kwa asilimia 100.

Katibu wa CCM Uenezi Wilaya ya Same Ndg. Mohamed Ifanda, ameipongeza Serikali kwa kutoa fedha za ujenzi wa daraja hilo pamoja na uongozi wa wilaya kwa usimamizi madhubuti wa mradi.

## VIJANA WANUFAIKA NA PIKIPIKI ZA MKOPO USIO NA RIBA.



***Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Same Bwa Charles Anatoly (aliyesimama) akiwapa nasaha vijana baada ya kupatiwa pikipiki za mkopo.***

Halmashauri ya Wilaya ya Same imetoa pikipiki 10 kwa vikundi vya vijana wajasiriamali kupitia mkopo wa asilimia kumi unaotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Akizungumzia Mkopo huo Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Same Bw.Charles Anatoly amesema Pikipiki hizo zilizotolewa zina thamani ya Shilingi Milioni 30 na zinatarajiwa kutumika kibiashara kama bodaboda.

Vikundi vilivyonufaika na Mkopo huo ambao ni sehemu ya Mkopo wa asilimia 10 uliitolewa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2025/2026 ni Kikundi cha Vijana Bodaboda Ndungu na
Kikundi cha Vijana Bodaboda Same.

"Katika robo hii ya kwanza tumetoa Mkopo wa Shilingi Milioni 184.5 na hizi Pikipiki tulizokabidhi leo ni sehemu ya Mkopo huo"Alisema Bw. Charles

Hata hivyo amewataka vijana hao kuhakikisha kuwa wanatumia Pikipiki hizo kwa malengo tarajiwa ili waweze kurejesha mkopo huo.

Bw.Charles pia amewakaribisha waombaji wengine wa Mkopo kuanza kuwasilisha maombi yao ya Mkopo kwani tayari dirisha la maombi limefunguliwa Novemba 05,2025 na litafungwa  Desemba 20,2025.

**WENYEVITI WA MITAA WAKUMBUSHWA KUFANYA VIKAO VYA KISHERIA.**



***Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo Same Bw.Uledi Lusasi akizungumza kwenye kikao Cha Baraza la mji mdogo Same,Kusoto ni Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo Bw.Ramadhani Mangare.***

Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo Same Bw. Uledi Lusasi amewakumbusha Wenyeviti wa Vitongoji  kuhakikisha kuwa wanafanya mikutano ya Vitongoji ili kujadili masuala ya Maendeleo ikiwa ni pamoja n a kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi.

Bw.Lusasi alitoa ushauri huo kwenye kikao cha Baraza la Mamlaka ambapo alisema vikao hivyo ambavyo vipo kisheria  ni muhimu vifanyike kwani ndivyo vinavyowaunganisha wananchi na Serikali yao.

Aidha amewataka Wenyeviti hao kusimamia Amani na utulivu katika maeneo yao na iwapo atatokea mtu wanayemtilia shaka watoe taarifa mapema kwenye Mamlaka husika ili hatua stahili ziweze kuchukuliwa.

“Nyie ni walinzi wa Amani kwenye maeneo yenu, hivyo basi kwenye Mtaa wako akiingia mgeni ambaye mnamtilia shaka hakikisheni mnatoa taarifa ili hatua stahili ziweze kuchukuliwa” alisema

**DC KASILDA AZITAKA TAASISI ZA SERIKALI KUTATUA KERO ZA WANANCHI**

Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni ameongoza kikao Cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) na kusisitiza Taasisi za Serikali kutatua kero na changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi ili kuboresha utoaji wa huduma.

Maelekezo hayo yametolewa na Mhe. Kasilda ameyatoa wakati akizungumza katika kikao hicho cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya ya Same (DCC) kilichofanyika wilayani hapa Disemba 08, 2025.

“Ninaielekeza kila taasisi kuhakikisha inasimamia kikamilifu majukumu yake. Wananchi wanahitaji huduma bora, tunawajibu wa kusikiliza na kutatua changamoto zao kwa wakati na kwa ufanisi.”

Aidha, amezitaka taasisi za serikali kushughulikia taarifa zinazotolewa na wananchi kwa haraka, hususan taarifa zinazohusu uharibifu wa miundombinu ya kimaendeleo na kijamii ikiwemo maji, umeme, barabara na maeneo mengine yenye athari kwa ustawi wa wananchi.

Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) ndiyo chombo muhimu kinachowakutanisha wataalamu, wadau na viongozi kupanga mikakati ya maendeleo, kufuatilia utekelezaji wa miradi, na kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika kwa manufaa ya wananchi.

**VIJANA KATA YA MAORE WAPATIWA ELIMU YA MIKOPO.**

Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Same Bw.Charles Anatoly akitoa Elimu kwa Vijana wa Kata ya Maore juu ya taratibu za kifuata ili kupata mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri.

Mikopo hiyo ambayo hutolewa kwa Wanawake,Vijana na watu wenye Ulemavu inatokana na asilimia 10 ya mapato ya Halmashauri na haina riba.

Amesema hatua muhimu za kufuata ili kupata mikopo ni kama ifuatavyo:-

Kuanziasha kikundi cha watu wasiopungua watano (wanaoaminiana).
Kutengeneza Katiba ya Kikundi.
Kusajili Kikundi wenye tovuti ya Wezesha Portal.
Kufungua Akaunti Benki.

Amesema baada ya kufuata hatua hizo Kikundi kitathibitishwa na baada ya kuthibitishwa wataweza kuomba Mkopo.

Afisa Maendeleo huyo alisema Mafunzo hayo ni sehemu ya Mafunzo ambayo hutolewa mara kwa mara kwa wananchi ili kuwawezesha kunufaika na Mkopo huo.

Sambamba na elimu ya mikopo pia vijana hao walielezwa kuhusu umuhimu wa kuilinda amani na kujiepusha na vitendo vya kihalifu.



**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**

**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**S.L.P 138, SAME**

**Mhariri wa Mkuu: Jimson Mhagama**

**Mhariri wa Habari: Amina Sangawe**

***Desemba, 2025 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz SAME DC samedc2022***